

# KS KIDSPORT

UP TO  
**\$150**  
TOWARDS CLUB  
FEES FOR KIDS!



## Je! Watoto wako wanataka kucheza michezo?

Programu ya Kidsport inatoa msaada mpaka wa \$150 kila mtoto kila mwaka kwa watoto ambao wanastahili kupata msaada wa kulipa ada za klabu ili kujiunga klabu ya michezo na kuanza kufurahia.


Michezo ni muhimu katika maendeleo ya mtoto: inaweza kusaidia kuboresha kujiamini kwake na kutoa njia yenye afya ili kufurahia shughuli za kimwili pamoja na marafiki yake.

Idara ya Serikali la Mtaa, Michezo na Tasnia za Kitamaduni inatia moyo watoto kwa nguvu ili kuhusika katika michezo ya jamii, siyo kwa faida pekee ya kimwili, ila pia kwa sababu ya matokeo mazuri kwa ustawi wa kiakili na kihisia wa watoto.

### Nani aweze kuomba?

Watoto wote wa Australia Magharibi wa umri wa miaka 5 hadi 18 ambao wameandikiwa kwa Kadi ya Kutunza Afya au Kadi ya Diskaunti ya Wenye Pensheni ya sheria halali (ona sampuli zinaonyeshwa chini) wanaweza kuomba. Kwenda tu kwenye:

[www.dlgsc.wa.gov.au/kidsport](http://www.dlgsc.wa.gov.au/kidsport)



Klabu anapoweza mtoto kutumia vocha yake pale panaweza kugunduliwa kwenye tovuti yetu

<https://kidsport.dlgsc.wa.gov.au/find-a-club>



Ikiwa unahitaji msaada kwa kuomba kwa gharimia hii, tafadhali tuma baruapepe kwa timu ya Kidsport kwa [kidsport@dlgsc.wa.gov.au](mailto:kidsport@dlgsc.wa.gov.au) au pigia simu +61 8 9492 9911. Ofisi ya manispaa ya eneo lako, shule, klabu au mtu wa mawasiliano ya jamii lako wanaweza pia labda kukusaidia na ombi lako.